**Title: Under the Mango Trees**

**EPISODE 10**

**Author: Romie Singh**

**Editors: Susanne Fuchs, Katrin Ogunsade, Maja Braun**

**List of characters for episode 10:**

- Narrator
- Desirée
- Bongo
- Eric
- Lorraine
- Endurance
- Babu
- TV voice
- April
- Family members in background

Karibu katika kisa cha mwisho cha mfululizo wa sehemu kumi za mchezo kwa jina Chini Ya Miembe, wenye Noa Bongo Jenga Maisha Yako. Mchezo huu unaangazia maswala ya uzazi wa mpango.
Katika sehemu hii ya mwisho Lorraine anahitajika kuanza kupanga mipango ya usoni, nae Desirée anjikuta kuwa mambo mengi yanamkabili kwa wakati mmoja.

SIG.TUNE UP HOLD UNDER AND FADE

**NARRATOR:** Uja uzito wa Lorraine sasa una wiki sita na angeweza kuficha hali yake hii katika mashindano ya pop idols lakini alionelea sio jambo jema kuwaficha waamuzi wa mashindano hayo na walimu wake pia kwa hivyo ameamua kulikabali swala hilo. Bongo alijisikia mtulivu baada ya kupigiwa simu na Lorraine. Msichana huyo hakuwa na habari kabisa kwamba kutokea mwanzo chaguo la Bongo lilikuwa ni Desirée ashiriki katika mashindano hayo ya Pop Idols. Hata hivyo mpaka sasa, Desirée hajatia saini mkataba bado na Bongo alikuwa na wasiwasi kwamba huenda akakataa kwa sababu ya majukumu ya kifamilia aliyonayo. Bongo ameamua kwenda katika kijiji cha Mtelera, kumtia shinikizo Desirée.

**Sc. 1 Interior**

FADE IN DIALOGUE

1. BONGO: Kuna kila dalili za kuonyesha kuwa wewe utafanikiwa katika mchujo wa kwanza, Des. Kitu gani kinachokuzuia kusema NDIO?

2. DESIRÉE: Nina wasiwasi sana, sijawahi kuimba mbele ya watu katika maisha yangu, na hasa ukizungumzia kuhusu mambo ya Radio na Televisheni - oh Mungu wangu wee!

3. BONGO: Usiwe na wasiwasi! Mimi ninaweza kukusaidia, yaani, kukupa mazoezi, kwanza jinsi ya kuwakabili watu, halafu

namna ya kuishika Maikrofoni, ile miondoko na kadhalika. Tuna wiki mbili bado na shule zimefungwa. Kwa hivyo tunahitaji kupanga kila kitu.

4. DESIRÉE: Hata sielewi kwa nini Lorraine alijitoa. Eric pia hajui sababu. Je wewe hakukwambia kitu chochote?

5. BONGO: Aliniambia lakini ni siri, Des. Mimi nafikiri ingekuwa bora kama wewe mwenyewe ungemuuliza. La muhimu ni, mimi nataka utie saini huu mkataba. Je utafanya hivyo?

6. MUSIC UP

**NARRATOR:** Desirée alivuta pumzi ndefu. Alijua kuwa kwanza ni lazima ampate baba yake na mjomba wake. Ilibidi lazima wamsaidie kuwalinda watoto. Bila msaada wao hangeweza kufanya lolote. Alivuta tena pumzi ndefu, halafu akautia saini mkataba. Kwa Lorraine, shida ya pili iliyomkabili ni shule. Lorraine tayari alikuwa ameshamueleza kila kitu nduguye pacha, Eric, nae alimuahidi kuwa atakuwa nae wakati wote na sasa Lorraine aliinua simu tayari kumpigia mwalimu mkuu, bwana, Adams. Japo alikuwa likizoni lakini Lorraine alitka kumuuliza iwapo angeweza kuendelea na masomo yake hadi amalize? Kwani mitihani ilitakiwa kuanza baada ya wiki chache tu.

**<u>Scene 2 On the phone</u>**

| | |
|---|---|
| 7. LORRAINE: | Mwalimu Adams. Mimi ni mwanafunzi wa darasa la12.....Ndio mwalimu.....Ninajiandaa kufanya mtihani wa mwisho katika miezi mitatu ijayo...lakini um... Nimegundua kuwa nina ujauzito wa wiki sita sasa...... Ndio mwalimuYes .......Je. unazungunmzia kuhusu sheria za shule? Ndio mwalimu...na unasema kuwa msichan mwenye mimba hawezi kuvumiliwa kabisa hapo shuleni? .......Eti? Utanifukuza shule? (gasps) Yaani siwezi kurudia masomo hata baada ya mwaka mmoja? Haiwezekani kabisa? Kwaheri, Mwalimu mkuu. (Bursts out crying) Nitafukuzwa shule. Hiyo itaniharibia kabisa ripoti yangu! Oh, Eric...sasa nitafanya vipi mtihani wangu? Au nitaingia vipi chuoni? |
| 8. ERIC: | Lorraine, dada yangu–shhh. Nasikitika kuwa hivyo ndivyo shule zinavyofanya. Maelfu ya wasichana duniani kote hulazimika kuacha shule kwa sababu wamepata ujauzito. |
| 9. LORRAINE: (sobbing) | Ameniambia kuwa mimi nitakuwa mfano mbaya kwa wasichana wengine |

hapo shuleni. Mwaka jana wasichana watano walipata mimba shuleni kwetu. Aliwafukuza wote. Anasisitiza kuwa lazima sisi tuwe funzo kwa wasichana wengine.

10. ERIC: Nadhani angeifanya shule yake kuwa mfano wa maendeleo. Shule ambayo wasichana wanapewa fursa ya kuendelea na elimu hadi wamalize japo kwa kuhudhuria  masomo ya jioni au labda wangeweza kukubaliwa warudi shuleni baada ya mwaka mmoja. Kwani hatutaki wanawake waelimike? Na kwa nini baba mtoto hapewi adhabu! Msichana anafukuzwa. Mvulana anakuwa huru.

11. LORRAINE: Ni kweli lakini halikuwa kosa la Sazi mimi ndie nimejiachia nikapata mimba, Eric.

12. ERIC: Pengine, lakini mimi naona hata yeye anahusika.  Hilo ni funzo kwetu sisi wanaume, hatuwezi tu kumwachia mwanamke peke yake ndio afuatilie maswala ya kinga ya uzazi. Naona kuwa ikiwa mvulana hataki matata basi atalazimika kutumia Kondom kila mara.

Ukweli ni kwamba kuna magonjwa ya zinaa, kuna virusi vya HIV, lazima mtu afikirie.

13. MUSIC UP

**NARRATOR:** Lorraine alimpigia simu Desirée. Akamweleza sababu ya kutokushiriki kwake katika mashindano ya Pop Idols. Ilikuwa vigumu kwa Desirée kuamini aliyo yasikia kutoka kwa rafiki yake. Lorraine, ana mimba? Alisikitika sana, Lakini Lorraine alikuwa mtulivu na kumtakia Des ushindi katika Pop Idols! Na kwa niaba yake, Des aliahidi kushiriki kwa bidii zake zote. Mshale wa saa ulikuwa unasonga mbele! Alihitajika kumpata baba yake mzee Babu kwanza halafu ampate mjomba wakeBlessing pia, alitaka kuwaambia wawachukue watoto wao haraka. Alikuwa amebakiwa na siku tano tu kabla ya mashindano. Eric alianza safari kwa gari yake pamoja na Des, na Endurance kwa lengo la kuwatafuta baba na mjomba wao.

**<u>Sc.3 In the car driving</u>**

14. ENDURANCE: Alama ile pale! Alama ya Kibluu pale mkono wa kulia! Ona imeandikwa Gereji ya Babu.

15. ERIC: Umeing’amua haraka Endurance asante! Sasa nitaegesha gari hapa.

16. FOOTSTEPS ON STREET; TRAFFIC.

In the workshop **SFX: hammering**.

17. DESIRÉE: Hivi ni viatu vya baba, mwangalie Yule pale chini ya gari. Mimi ninavijua! (shyly) Baba?

18. ENDURANCE: (louder) Baba! Ni sisi, Endurance na Desirée.

19. **SFX:** heavy groaning as Babu pulls himself out from under the car

20. BABU: Hah! (Embarrassed laughing) Endurance! Desirée!

21. DESIRÉE: (relieved) Baba! Oh, Nimefurahi sana tumekupata!

22. BABU: Ni ajabu gani hii jamani! Na huyu ni mtoto wa daktari Alice, Eric, sio?

23. ERIC: Ndio, mzee!

24. BABU: Siwezi kuwapa mkono kwani mikono yangu imejaa mafuta. Karibuni. Twendeni ofisini kwangu tukazungumze!

25. **SFX:** Background radio music/ chairs scraping.

26. DESIRÉE: Baba gereji yote hii ni yako?

27. BABU: Ndio, niliinunua baada ya kuliuza shamba letu, japo kuwa nyanya yenu Linda hakunitaka kabisa kwa hivyo sikutaka kuja nyumbani hadi pale nitakapokuwa nimeinuka vizuri kibiashara. Hata hivyo nilitaka kuwapigia simu katika siku hizi hizi – kweli tena.

28. DESIRÉE: (hard) Ni kitu gani kilichokukataza kutupigia?

29. ENDURANCE: Baba unaishi wapi?

30. BABU: (coughing embarrassed) I... um… naishi na… Maryam.

31. ENDURANCE/DESIRÉE: (shocked) Maryam?

32. BABU: Ndio na watoto wake wawili.

33. DESIRÉE: Yaani baba ulituacha muda mfupi tangu mama alipofariki –kumbe ulikuwa unakuja huku kuishi na mwanamke mwingine na watoto wake? Na sisi je? Watoto wako? Baba, uliweza vipi kufanya namna hiyo? Umemjua kwa muda gani huyo Maryam, uh? Kwa

muda gani? (Sobbing through next part of dialogue)

34. BABU: (stuttering) Mamaa… mama yenu na mimi ....Nili ....nili **(Suddenly angry)** Desirée, sina haja ya kukujibu swali hilo. Lakini nilipanga kuwa ningewachukuwa mje muishi nami baada ya kupata nyumba kubwa. Ndio maana nafanya kazi kwa bidii.

35. ERIC: (comforting) Shh, Des. Najua huna raha! Lakini ni lazima tumuulize baba yako kuhusu…

36. DESIRÉE: (Sniffing/more controlled) Ndio.. Baba, hatuna muda wa kutosha ningependa kukuuliza kama Endurance anaweza kuja kukaa nawe japo kuwa mara kwa mara mwishoni mwa wiki. Kwa mfano mwisho wa wiki ijayo?

37. ENDURANCE: Tafadhali baba?

38. BABU: Kwa kweli sijui. Lazima nimuulize kwanza Maryam.nina… nataka ni…

39. DESIRÉE: Baba, sisi ni watoto wako. Nadhani ungetupa kipaumbele.

40. BABU: Ndio, ni kweli, um… nadhani hakuna matatizo, lakini kama Endurance uko tayari kulala pamoja na mtoto wa Maryam, ana miaka tisa.

41. ENDURANCE: (happy) ndio baba!

42. ERIC: Hutajuta mzee, Unamsaidia mwanao wa kike kuwa nyota.

43. BABU: Nafahamu! Meneja wako Bongo, amenipigia simu . Amekusifu sana na ana matumaini makubwa kwako. Des, nisamehe sana, lakini (Laughing)kama msaada wangu utakufanya ushinde milioni. Basi nitafanya lolote!

44. ENDURANCE: Halafu atapata pesa nyingi, atanunua nyumba kubwa na sote tutaishi pamoja! Hata wewe, Eric!

45. DESIRÉE: (embarrassed) Endurance!

46. ERIC: (laughing) Sawa sawa! (Seriously) Oh, jambo jingine, je unafahamu mjomba Blessing yuko wapi?

47. BABU: Ndio, tunafanya kazi ya kutengeneza magari pamoja. Atakuja sasa hivi tu.

48. DESIRÉE: Oh, wow! Hata siamini!

49. **SFX:** MUSIC. FADE UNDER

**NARRATOR:** Mjomba Blessing nae alikuwa ameshajipatia mke mwingine ambae pia alikuwa na watoto. Yeye alipanga kuwa watoto wake waendelee kuishi na nyany Linda. Hiyo ilikuwa nafuu kubwa kwake. Usiku wa kuamkia siku ya mashindano ya Pop Idols, Endurance na familia mpya ya baba yake walikaa pamoja kuangalia mashindano hayo kwenye televisheni. Eric, Lorraine, mama yao na Sazi nao walikuwa nyumbani pamoja wakimtakia heri zote za ushindi. Familia kubwa ya Desirée yenye mchanganyiko wa vizazi vitatu nayo ilikuwa pamoja! Bella na mpenzi wake Robert walimualika nyanya ili wayaangalie mashindano hayo kwenye Televisheni pamoja, Kila mmoja alishikwa na kiwewe pale Desirée alipopanda jukwaani na kuimba kwa sauti tamu kama ya ndege!

50. DESIRÉE: Habari za jioni. Ufuatao ni wimbo ambao mama yangu alipenda sana kuuimba.Wimbo huu ninamtunukia rafiki yangu wa dhati, Lorraine!

51. LORRAINE (at home) Oh, Des, asante sana-, Rafiki yangu!

52. **SFX:** Live applause from family members. PLUS TV audience applause

53. ALL: (different moments)lo. Ni mrembo kweli...angalia nguo nzuri alizovaa… Shhh...hata siamini kuwa Yule ni Des wetu! Amekua jamani!

54. SIG TUNE (Desiré singing)

55. **SFX:** Applause.

56. TV VOICE: Desirée Thomas,umechagulia kuendelea mbele!

57. **SFX:** FADE UP SINGING/CHEERING. HOLD UNDER

**NARRATOR:** Chini ya Miembe upepo mwanana wa jioni ulikuwa ukipeperusha majani. Maembe yalikuwa tayari yamekomaa na yanasubiri kuanza kudondoka. Bila shaka miti mipya ya miembe ingeota mahala pale siku moja. Kama ungesikiliza kwa makini, ungeisikia sauti ya Bi, April akinong'ona kwa watoto wake aliowatoka. Watoto ambao aliwapa maisha yake yote.

58. APRIL: Bella, Desirée, Endurance, nawatakia Baraka katika maisha yenu ya usoni. Maisha yako ni yako (echo) ini maisha yako..ni maisha yako.....

SIG. TUNE UP

**OUTRO:**

Na hiyo ndio ilikuwa sehemu ya kumi nay a mwisho katika NOa Bongo Jenga Maisha Yako kwenye mfululizo wa mchezo wa hadithi kwa jina “Chini Ya Miembe.” Mchezo huu wa redio umeandikwa na Romie Singh. Ni matumaini yetu kuwa umejifunza mengi kuhusu njia za uzazi kwa mpango na jinsi njia hizo zinavyio weza kukusaidia kuimarisha maisha yako.Wasichana na wapenzi wao wanafursa ya kufanya maamuzi yenye faida kwao katika swala zima la mapenzi au ni wakati gani wangetaka kuwa na familia.

Kumbuka unaweza kuusikiliza tena mchezo huu au michezo iliyotangulia. Waambie marafiki zako pia kuhusu Noa Bongo Jenga maisha yako. Tutafurahi pia kupokea maoni yako. Anuani ya mtandao wetu ni: d w world dot d e mkwaju I b e.

Asante kwa kuwa nasi. Kwaheri, na ubaki salama.

**END OF EPISODE TEN**